JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

# UTEKELEZAJI WA MPANGO WA UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA (BLUEPRINT) KATIKA SEKTA YA KILIMO




Agosti, 2020

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

# UTEKELEZAJI WA MPANGO WA UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA (BLUEPRINT) KATIKA SEKTA YA KILIMO

AGOSTI, 2020

# UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA KATIKA KILIMO MAZAO KAMA SEHEMU YA UTEKELEZAJI WA BLUE PRINT

# 1. UTANGULIZI

Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija ya mazao. Katika kutimiza lengo hilo, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kwa dhati kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa kupitia Sera na sheria za kilimo. Maboresho ya Kodi, Tozo na Ada katika kilimo yamenufaisha wakulima, kwa sababu baadhi ya tozo hizo hutozwa moja kwa moja kwa wakulima hivyo kupunguza mapato yao.

Aidha, baadhi ya Kodi na Tozo zinazotozwa kwa wafanyabiashara zimekuwa zikiathiri ushindani wa mazao ya Kilimo kwenye soko kwa kuwa huongeza gharama za ufanyaji biashara. Hali hiyo husababisha wafanyabiashara kurudisha gharama hizo kwa wakulima kwa kupunguza bei za mazao wanazolipa kwa wakulima.

Serikali katika kipindi cha miaka mitano (5) pamoja na mambo mengine imefanya maboresho ya Kodi, Ada na Tozo mbalimbali katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo sekta ya kilimo (mazao). Maboresho hayo ni matokeo ya utekelezaji wa Programu ya kuendeleza Sekta ya kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) hususan eneo Kuu la Nne linalohusu kuweka mazingira wezeshi ya kuendeleza Sekta ya kilimo na kuwezesha Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini na vilevile utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*).

# 2. MABORESHO YALIYOFANYIKA KATIKA KILIMO MAZAO

**Katika kipindi cha miaka mitano Serikali imefanya marekebisho mbalimbali katika sekta ya kilimo hususan sekta ndogo ya kulimo kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara.**

**Miongoni mwa marekebisho hayo ni maboresho ya mfumo wa Kodi, Ada na Tozo mbalimbali pamoja na marekebisho ya kimuundo na kimfumo kama ifuatavyo:**

## 2.1 MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA NA TOZO MBALIMBALI KATIKA KILIMO

Katika kipindi cha miaka mitano (5) Serikali imefanya maboresho ya ada na tozo kwa kufuta jumla ya tozo na ada 105 zilizokuwa zinatozwa na bodi na taasisi zilizo chini ya Wizara ya kilimo  kama ifuatavyo; kwa zao la tumbaku tozo kumi (10); zao la Kahawa tozo ishirini (20); zao la Sukari tozo kumi na saba (17); zao la Pamba  tozo nne (4); zao la Korosho tozo sita (6); zao la chai tozo tano (5); Tasnia ya mbegu zilifutwa tozo kumi na mbili (12); Tasnia ya mbolea tozo nne (4); Mfuko wa pembejeo tozo moja (1) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika tozo ishirini na sita (26).

Aidha, katika kipindi hicho Serikali pia ilipunguza viwango vya ada na tozo katika zao la tumbaku (2); mbolea moja (1); na kahawa moja (1).

### 2.1.1 Maboresho ya kodi kupitia sheria mbalimbali

Katika kipindi cha miaka mitano (5) Serikali imefanya marekebisho ya Sheria mbalimbali za kodi zinazohusiana na maendeleo ya mazao ya kilimo kama ifuatavyo.

**Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982**

Serikali imefanya Marekebisho katika viwango vya ushuru wa mazao (*produce cess*) kwa kupunguza kutoka asilimia 5 hadi 3 ya bei ya shambani (*farm gate price*). Aidha, kupitia marekebisho hayo mazao yasiyozidi tani moja yamesamehewa ushuru wa mazao wakati wa kusafirishwa kutoka wilaya moja kwenda nyingine.

**Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) SURA 148**

Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya VAT ili kuwawezesha wauzaji wa bidhaa nje ya nchi wakiwemo wauzaji wa bidhaa na mazao ya kilimo kuendelea kujirejeshea Kodi ya VAT (*Zero rated*) ili bidhaa hizo ziweze kushindana katika masoko ya nje. Hatua hiyo inalenga kuzingatia msingi wa utozaji wa VAT kwa kuzingatia mahali bidhaa inapotumika (*destination principle).*

**Ushirika**

Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato SURA 332, kwa kuongeza kiwango cha Mapato ghafi yasiyotakiwa kutozwa Kodi ya Mapato kutoka shilingi 50,000,000/= hadi shilingi 100,000,000/= kwa mwaka kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi. Lengo la hatua hiyo ni kutoa unafuu wa Kodi ya Mapato kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi

na vyama vya kuweka kukopa (SACCOS) kwa kuwa vyama hivyo vina mitaji midogo. Marekebisho hayo yamechangia kwa vyama vya ushirika kuwanufaisha wanachama wake kwa njia ya ongezeko la gawio na mikopo.

## Bima ya kilimo cha mazao



Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kutoa msamaha wa VAT kwenye huduma ya Bima ya kilimo cha Mazao. Lengo la msamaha huo ni kupunguza gharama na kutoa unafuu katika bima za kilimo ili kuwawezesha wakulima kuziwekea bima shughuli za kilimo na pia kuvutia wakulima wengi kutumia huduma za bima. Bima ya Kilimo ni muhimu kwa wakulima katika kujikinga na majanga mbalimbali yanayoathiri shughuli za kilimo ikiwemo ukame, mafuriko na magonjwa ya mimea.

## Zao la Zabibu

Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 10 hadi asilimia sifuri (0) kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa vifuniko vya chupa za mvinyo (*corks*) vinavyotambulika kwa HS Codes 4503.10.00 kwa kuwa havizalishwi nchini.

Lengo la maboresho hayo ni kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mvinyo ili kuhamasisha kilimo cha zabibu nchini pamoja na ajira. Aidha, utaratibu wa "*Duty Remission*" ndio utakaotumika kutoa unafuu huo.

## Zao la Chai

Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye chai inayoagizwa kutoka nje ya nchi na inatambulika kwa HS Codes 09.02. Lengo la maboresho hayo ni kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha kilimo cha chai nchini pamoja na kuongeza ajira katika mnyororo wa thamani wa zao la chai.

## Zao la Mkonge



Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 katika kipindi cha mwaka mmoja kwa magunia yanayoagizwa kutoka nje ya nchi *(sacks and bags of jute or other textile bast*

*fibers of heading* 53.03) yanayotambuliwa katika HS Codes 6305.10.00. Lengo la maboresho hayo ni kulinda viwanda vya ndani vinavyotengeneza magunia ya mkonge, kukuza na kuendeleza kilimo cha zao la mkonge pamoja na kuongeza ajira katika mnyororo wa thamani na katika pato la Taifa.

## Zao la Kakao

Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia sifuri (0) hadi asilimia 10 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa kakao inayoagizwa kutoka nje ya nchi na inayotambulika kwa HS Codes 1805.00.00. Lengo la maboresho hayo ni kuchochea na kuhamasisha kilimo cha zao la Kakao nchini na kuongeza mchango katika pato la Taifa.

## Zao la Kahawa

i). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga/kusindika kahawa nchini. Vifungashio hivyo vinatambulika kwa HS Codes 7310.21.00; 6305.10.00; 3923.50.10; 3923.50.90; 3920.30.90 na 48.19. Lengo la maboresho hayo ni kuongeza thamani ya zao la kahawa na kutoa unafuu

wa gharama uzalishaji kwa viwanda vinavyosaga/ kusindika kahawa nchini. Aidha, utaratibu wa *"Duty Remission"* utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo.

ii). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye Kahawa inayoagizwa kutoka nje ya nchi inayotambulika kwa (HS Code 09.01). Lengo la Maboresho hayo ni kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha kilimo cha kahawa nchini ili kuongeza Ajira na mapato ya Serikali.

## Zao la Korosho



Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri (0) kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa vifungashio vya kuhifadhia korosho, vinavyotambulika kwa HS Codes 3923.21.00.

Lengo la Maboresho hayo ni unafuu wa gharama za uzalishaji kwa viwanda vya kubangua korosho nchini na hivyo

kuchochea uongezaji wa thamani kwa zao la Korosho ndani ya nchi. Aidha utaratibu wa "*Duty Remission*" utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo.

## Zao la Pamba



Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri (0) kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia pamba, vinavyotambulika katika HS Codes HS codes 3920.30.90; 6305.39.00 na 7217.90.00.

Lengo la maboresho hayo ni kuvutia uwekezaji zaidi katika viwanda vya kuchambua pamba ili kuchochea uongezaji wa thamani kwa zao la pamba nchini.

## Zao la Miwa/Sukari

i). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya kiwango cha asilimia 100 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa sukari ya matumizi ya kawaida (*consumption sugar*) inayoagizwa kutoka nje

ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (*Gap sugar*) ya uzalishaji wa sukari nchini.

ii). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya tasnia ya sukari kwa Kupunguza kiwango cha tozo inayotozwa na Bodi ya Sukari (*Sugar board import fee*) kutoka asilimia 2 ya thamani ya mzigo au asilimia 2 ya dola za Marekani mia nne na sitini (460) sawa na takriban dola za Marekani 9 kwa tani, chochote kitakachokuwa kikubwa hadi dola 7.5 kwa tani moja.

## Mazao ya Bustani



i). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha wa kiwango cha asilimia sifuri (0) kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 10 kwenye makaratasi yanayotambulika kwa (HS Codes 4805.11.00 na 4805.19.00) na kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa makaratasi yanayotambulika kwa (HS Code 4805.24.00 na 4805.25.00). Aidha, utaratibu wa "*Duty Remission*" utatumika ambapo viwanda vinavyotengeneza

vifungashio hivyo ndivyo vitakavyonufaika. Lengo la maboresho hayo kutoa ni unafuu kwa wazalishaji wa vifungashio vya mazao ya mbogamboga ili kuwawezesha wakulima kupata vifungashio nchini ambavyo kwa sasa vinaagizwa kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa.

ii). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa bidhaa za mazao ya bustani (*Horticultural Products*) zinazotambulika kwa HS Codes 0603.11.00; 0603.12.00; 0603.13.00; 0603.14.00; 0603.19.00; 0604.20.00; 0604.90.00; 0701.90.00; 0702.00.00; 0703.10.00; 0703.20.00; 0706.10.00; 0710.10.00; 0710.21.00; 0710.22.00; 0710.30.00; 0714.10.00; 0714.20.00; 804.30.00; 0804.40.00; 0804.50.00; 0805.10.00; 0805.40.00; 0805.50.00; 0806.10.00; 0807.11.00; 0807.20.00; 0808.10.00; na 0808.20.00. Lengo la maboresho hayo ni kulinda wakulima wa ndani ili kuendeleza kilimo cha mbogamboga na maua hapa nchini.

iii). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa nyanya zilizosindikwa ambazo zinaagizwa kutoka

nje ya nchi na zinatambulika kwa HS Codes 2103.20.00. Lengo la maboresho hayo kulinda viwanda vya ndani kuimarisha soko la zao la nyanya kwa wakulima.

## Mbegu za Mazao ya Kilimo



i). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia sifuri (0) badala ya kiwango cha awali cha asilimia 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa vifungashio vinavyotambulika kwa (HS Codes 3923.29.00; 6305.10.00; 4819.40.00,7310.29.90; 6305.33.00; 6305.20.0; 6304.91.90; 7607.19.90). Utaratibu utakaotumika kutoa unafuu huo ni wa "*Duty Remission*". Lengo la maboresho hayo ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbegu hapa nchini na hivyo kuongeza uzalishaji wa mbegu.

## Mafuta ya Kula

i). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika uagizaji wa mashine na mitambo kwa wazalishaji wa mafuta ya kula yanayotumia mbegu zinazozalishwa nchini kama Alizeti, Ufuta, Karanga, Pamba na Michikichi kwa lengo

la kuhamasisha uwekezaji katika usindikaji/ukamuaji wa mafuta yatokanayo na mbegu za mazao ya kilimo.



ii). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia sifuri (0) kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa mafuta ghafi ya kula (alizeti, mawese, soya, mizeituni, nazi,karanga, mahindi) yanayoagizwa kutoka nje ya nchi ambayo yanatambulika kwa HS Codes 1507.10.00; 1508.10.00; 1511.10.00; 1513.11.00; 1514.11.00; 1514.91.00; 1515.11.00. Serikali kuendelea kutoza kiwango cha asilimia 25 badala ya kiwango cha asilimia 10 kwa mafuta ghafi yanayotambulika kwa HS Codes 1512.11.00; 1515.21.00;1515.30.00. Lengo la maboresho hayo ni kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta hapa nchini na kuongeza ajira viwandani na mashambani pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi;

iii). Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa mafuta ya kula (Alizeti, Mawese, Soya,

Mizeituni, Nazi, Karanga na Mahindi) yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati na cha mwisho (semi-refined and refined/double refined oil) ambayo yanatambulika kwa HS: Codes 1507.90.00; 1508.90.00; 1509.90.00; 1510.00.00; 1511.90.10; 1511.90.30; 1511.90.90; 1512.19.00; 1512.29.00; 1513.19.00; 1513.29.00; 1514.19.00; 1514.99.00; 1515.19.00; 1515.29.00; 1515.50.00; 1515.90.00. Lengo la maboresho hayo ni kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta hapa nchini na kuongeza ajira viwandani na mashambani pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi;

### 2.1.2 Ada na tozo za taasisi za udhibiti



Katika kipindi cha miaka mitano (5) Serikali imefanya marekebisho ya Sheria mbalimbali za taasisi za udhibiti kwa lengo la kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na wawekezaji nchini. Tozo na Ada zilizofutwa au kupunguzwa zinasimamiwa na Taasisi za OSHA, Tume ya Ushindani, Bodi za mazao, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Tozo na Ada

hizo zilizofutwa zinatarajiwa kuleta unafuu kwa wawekezaji wa sekta ya kilimo kwa kuwa zimekuwa zikilalamikiwa na wawekezaji katika sekta ya kilimo kama ilivyo kwa wawekezaji wa sekta nyingine za uchumi.

## 2.2 MABORESHO YA MIUNDO NA MIFUMO KATIKA KILIMO MAZAO

### 2.2.1 Kupunguza Idadi ya Taasisi za Udhibiti



Katika jitihada za kupunguza taasisi za Serikali ambazo zilionekana kuwa na shughuli zinazofanana, Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kikao chake cha tarehe 19 Mei, 2020 lilipitisha kutungwa kwa Sheria ya Viuatilifu na Afya ya Mimea ya Mwaka 2020 ambayo imeshasainiwa na Mhe. Rais na hivyo kuwa Sheria rasmi. Sheria hiyo imefuta Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Ukanda wa Kitropiki (Tropical Pesticide Research Institute-TPRI Act) Na. 18 ya mwaka 1979 na Sheria ya Hifadhi ya Mimea (Plant Protection Act- PPA) Na. 13 ya Mwaka, 1997 na kuanzisha Mamlaka ya Viuatilifu na Afya ya Mimea ambayo imeundwa kutokana na muunganiko wa Sehemu ya Afya ya Mimea iliyokuwa Wizarani chini ya Idara ya Maendeleo ya Mazao na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Ukanda wa Kitropiki.

### 2.2.2 Mifumo ya Kidigitari Katika Wizara ya Kilimo

Wizara ya Kilimo imeweka mifumo ya kidigitari kwa ajili ya sababu zifuatazo;

a) Kurahisisha ufanyaji biashara;
b) Kufuatilia mwenendo wa uagizaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo;
c) Kurahisisha huduma za utoaji wa vyeti vya usafi wa mazao yanayotoka nje ya nchi;
d) Kurahisisha huduma za utoaji vibali vya kuingiza au kuuza mazao ya kilimo nje ya nchi;
e) Huduma za utoaji wa leseni za biashara ya mazao zinazotolewa na Bodi za mazao;
f) Usajiri wa wakulima ili kuwatambua kwa ajili ya wepesi wa utoaji huduma za mikopo, pembejeo na ugani;
g) Kurahisisha utoaji wa huduma za ugani na kuwaunganisha wakulima na wanunuzi wa mazao kwa kutumia fursa za sasa kama Simu kitochi, simu janja na kompyuta;
h) Kutoa taarifa za utekelezaji kwa Wizara zinazopima mafanikio ya viashiria vya malengo ya Wizara;
i) Kurahisisha kuwatambua na kuwasajili wadau wa kilimo kama wadau wa Maendeleo, taasisi za kiraia zinazojishughulisha na kilimo, wasindikaji na watoa huduma wengine;
j) Kusajili mawakala na wazalishaji wa mbegu kurahisisha utambuzi na utoaji wav yeti na leseni;
k) Kuzuia matumizi ya mbegu zisizo na ubora na viuatilifu visivyo na ubora

## *Mifumo Iliyopo Kwa Sasa Ni Kama Ifuatavyo (Inayotumika)*

### i) Agricultural Trade Management Information System (ATMIS).

Mfumo huu unatumika kutoa huduma za utoaji vyeti vya usafi wa mazao ya mimea yanayotoka nje ya nchi, utoaji wa vibali vya kuingiza au kuuza nje mazao ya mimea, utoaji wa vibali na leseni za biashara zinazotolewa na Bodi za Mazao pamoja na baadhi ya Taasisi za Wizara kwa njia ya kielektroniki. *https://atmis.kilimo.go.tz*

### ii) Farmers Registration System

Mfumo huu unatumika kusajili wakulima wa mazao mbalimbali hapa nchini kwaa njia ya kielektroniki. Jumla ya wakulima 1,325, 798 wa mazao yanayosimamiwa na Bodi wamesajiliwa kati ya wakulima 1,447,239 sawa na asilimia 91.6. Usajili wa wakulima wa mazao mengine unaendelea. *http://frs.kilimo.go.tz*

### iii) E-Extension Services (Mobile Kilimo)

Mfumo huu ni wa kielektroniki, unatumika kuwaunganisha wakulima na wanunuzi wa mazao yao na vilevile unatumika na Mabwana/Mabibi shamba kutoa huduma za ugani kwa wakulima kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia simu za kitochi, simu janja na kompyuta. *http://exts.kilimo.go.tz*

## iv) Mfumo wa Kutunza Takwimu za Sekta ya Kilimo (Agricultural Routine Data System-ARDS)

Mfumo huu unatumika kutunza taarifa na takwimu za sekta ya kilimo, anuani ya mfumo huu ni *https://ards.kilimo.go.tz*

## v) Mfumo wa Kusajili Wadau wa Kilimo (Tanzania Agriculture Stakeholders Database)

Mfumo huu wa kielektroniki unatumika kusajili wadau mbalimbali wanachangia katika sekta ya kilimo. Baadhi ya wadau wanosajiliwa ni pamoja wafadhili na miradi wanayofadhili, taasisi za kiraia na za kiserikali, watoa huduma, wasindikaji na wengine wengi wanaojihusisha na masuala mbalimbali katika sekta ya kilimo. Wadau wanatakiwa kujisajili wenyewe kwenye mfumo kupitia anuani ya *http://assb.kilimo.go.tz*

## vi) Mfumo wa Kuhabarisha Umma –Tovuti ya Wizara

Mfumo huu unatumika kuhabarisha umma kwa taarifa mbalimbali zinazofanywa na Wizara kila siku. Anuani yake ni *https://www.kilimo.go.tz*

## vii) Seed Dealers Registration System

Mfumo huu unatumika kusajili mawakala na wazalishaji wa mbegu hapa nchini. Mfumu unasaidia taasisi ya kuidhinisha mbegu hapa nchini (TOSCI) kusajili wadau wake.

## viii) Pesticide Management Information System

Mfumo huu unatumika kurahisisha shughuli za kiofisi na kibiashara kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huu unatumiwa na taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu (TPRI). Shughuli zote za kibiashara zinazofanywa na taasisi ya zinafanyika kwa njia ya kielektroniki ili kuboresha huduma kwa wateja wao.

*Kwa Mawasiliano:*
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA KILIMO**
**Mji wa Serikali, Mtumba, S.L.P. 2182, DODOMA.**
**Simu: +255 (026) 2321407 • Nukushi: +255 (026) 2320037**
**Barua pepe: ps@kilimo.go.tz • Tovuti: www.kilimo.go.tz**